



Maswali yanayoweza kuulizwa kwa usaili wa wasimamizi wa Sensa 2022

1. Explain what is SENSE/ Nini maana ya Sensa.

2. Difference between Longitude and Latitude.

i) Difference between Street and Road.

ii) Difference between House and Household

3. What is the method used to avoid COVID-19?

1. Eleza historia yako kwa ufupi.

2. Andika takwimu za namba 1 hadi 10.

3. Rais wa Tanzania anaitwa nani?

6. Barua ya kirafiki ina vipengele vingapi?

1. Mtendaji wako wa Mtaa anaitwa nani?

2. Mwemyekiti wako anaitwa nani?

3. Kata yenu ina vitongoji vingapi?

4. Diwani wako anaitwa nani?

5. Kata yako ina Mitaa mingapi?

6. Ofisi za Kata zipo mtaa gani?

Maswali yanayoweza kuulizwa kwa usaili wa wasimamizi wa Sensa 2022

1. Jielezee, wewe ni nani?

Hapa utajibu kutokana na taarifa zako binafsi ulizojaza wakati unafanya maombi kwenye mtandao.

2. Taja majina ya wadhamini wako

Hapo utataja majina ya wadhamini wako kama ulivyoandika kwenye mtandao wakati unafanya maombi.

3. Sensa hufanyika kila baada kipindi cha miaka mingapi?

Jibu: Kila baada ya miaka 10.

4. Sensa ya kwanza ilifanyika mwaka gani?

Jibu: 1967

5. Nini maana ya Sensa ya watu na Makazi?

Jibu: Sensa ya watu na makazi ni utaratibu wa kukusanya, kuchambua, kutathimini na kuchapisha na kusambaza takwimu za kidemographia, kiuchumi na kijamii kuhusiana na watu wote na makazi yao katika nchi kwa kipindi maalum. Kwa maana nyingine, sensa ni zoezi maalum lenye lengo la kupata idadi ya watu wote katika nchi, kwa umri na jinsia, mahali wanapoishi na hali yao ya elimu, hali ya ajira, hali ya vizazi na vifo na hali ya makazi.

6. Ni nini umuhimu wa Sensa ya watu na makazi?

Jibu: Umuhimu wa kipekee wa Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ni pamoja na:-

1. Kuisadia Serikali kupata taarifa za msingi zitakazosaidia mchakato wa utekelezaji wa Dira ya Maendeleo ya mwaka 2025, mageuzi ya masuala ya

- afya na jamii, pamoja na ufuatiliaji wa ajenda za maendeleo za kimataifa;
2. Taarifa za idadi ya watu husaidia katika mamlaka za wilaya katika utekelezaji wa mipango ya maendeleo ambayo huakisi matakwa ya watu katika ngazi husika na kusaidia kwenye uwiano wa mgawanyo wa rasilimali;
 3. Taarifa za msingi za hali ya kidemografia, kijamii na kiuchumi za idadi ya watu na makazi za mipango katika ngazi zote;
 4. Kigawio katika kukokotoa viashiria vingine mfano Pato la mtu mmoja mmoja, Pato la Taifa, Ajira na ukosefu wa Ajira na kiwango cha uandikishaji wa wanafunzi;
 5. Taarifa itakayoweza serikali kujua ongezeko la idadi ya watu, kwa mgawanyo na viashiria vingine, ambavyo ni muhimu kwa usimamizi wa mazingira; na
 6. Msingi wa utawala bora na ujumuishaji wa demokrasia. Takwimu sahihi za Sensa zinahitajika kwa ajili ya ugawaji wa majimbo ya uchaguzi kwa ufanisi, kurekebisha mipaka ya kiutawala katika serikali za mitaa.
 7. Sensa ya watu na makazi mwaka huu yatafanyika tarehe gani?

Jibu: Tarehe 23/08/2023

8. Zipi ni kazi za Karani wa sensa? (Kwa walioomba nafasi hiyo)

Jibu: Kazi za karani wa sensa ni;

1. Kutambua mipaka ya eneo la kuhesabia watu kwa kulinganisha na ramani ya eneo la kuhesabia watu na maelezo ya mipaka yaliyopo kwenye ramani hiyo ; Kushirikiana na msimamizi na uongozi wa eneo husika kutambua kama katika eneo la kuhesabia watu kuna makundi maalaum yanayotakiwa

kuhesabiwa kwa utaratibu maalum tofauti na kaya za kawaida ;

2. Kuhoji dodoso la jamii katika ngazi ya kitongoji/mtaa/shehia.

3. Kuhesabu watu wote waliolala ndani ya mipaka ya eneo la kuhesabia watu usiku wa kuamkia siku ya Sensa ndani ya muda uliopangwa.

4. Kutuma katika mfumo kazi zilizofanyika na kukamilika kila siku Makao Makuu ya NBS / OCGS.

5. Kuvitumia vifaa vyote na nyaraka za Sensa kwa kadiri ya malengo yaliyokusudiwa.

9. Zipi ni kazi za Msimamizi wa Maudhui? (Kwa walioomba nafasi hiyo)

Jibu: Kazi za msimamizi wa maudhui ni;

1. Kuhakikisha kuwa kila karani wa Sensa anatambua eneo la kuhesabia watu

2. Kuhakikisha kwamba kila karani ana vifaa muhimu kama ilivyoorodheshwa katika " Mwongozo wa Karani wa Sensa ".

3. Kuhakikisha kuwa makarani wameelewa kazi na ratiba zao zimeandaliwa vizuri na wanazifuata.